

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

SHULE YA SEKONDARI KYUU
S.L.P. 175
HAI
15/12/2020
SIMU:0754391093

Kumb.Na.KSS/JOIN/2021/VOL 1

Jina la Mwanafunzi.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYUU
WILAYA YA HAI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI



Nina furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari KYUU iliyopo KATA YA MASAMA MAGHARIEI mwaka 2021. Muhula wa kwanza wa masomo unanza tarehe 11/01/2021 SAA MOJA KAMILI ASUBUHI siku ya Jumatatu. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe tajwa bila kukosa.

2.0 MAHITAJI MUHIMU YA SHULE


a) SARE YA SHULE

WAVULANA: Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi na suruali mbili (2) za rangi ya **MOTO (KITAMBAA KIMEAMBATANISHWA)** upana wa suruali uwe nchi 15. Rangi ya sweta ifanane na rangi ya suruali. Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi vyenye kamba visiwe raba na visiwe na kisigino na soksi jozi mbili rangi nyeusi .Pia ashone tai inayofanana na rangi ya suruali.

Suruali (wavulana)





VIATU NA SOKSI



upana nchi 15



WASICHANA: Blauzi mbili (2) nyeupe na sketi mbili (2) rangi ya **MOTO (KITAMBAA KIMEAMBATISHWA)** Sketi iwe pana yenye marinda 16 (mbele marinda 8 na nyuma marinda 8) urefu ufike kwenye unyayo. Rangi ya hijab iwe rangi nyeupe. Rangi ya sweta la shule ifanane na rangi ya sketi, viatu jozi mbili (2) vya ngozi vyenye kamba visiwe na kisigino na soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe. Rangi ya tai ifanane na sketi.

Tafadhali mzazi zingatia rangi ya kitambaa (kilichoambatanishwa hapo juu) ili kuepusha usumbufu kwa mzazi.



NGUO ZA MICHEZO.

Wavulana: Bukta ya bluu isiyokolea (Aqua blue) na T/Shirt ya rangi bluu isiyokolea (Aqua blue) ya mikono mifupi.



Nguo za michezo kwa wavulana na wasichana ni track suit yenye rangi ya bluu isiyokolea (aqua) na t-shirt ya bluu.

Wasichana: Track suti rangi ya bluu isiyokolea na T/Shirt rangi ya bluu isiyokolea.



Pia awe na buti nyeusi wakati wa mvua tu (wasichana na wavulana)

VIFAA VYA TAALUMA

Daftari kumi (COUNTER BOOK) na daftari ndogo kumi za mazoezi, kalamu za bluu na mkebe wa hesabu (compass), rula, kamusi ya kiingereza iliyotafsiriwa kwa kiingereza (dictionary), penseli na ufuto. Begi imara la kubebea vifaa vya shule.

VIFAA VYA CHAKULA

Mahitaji na utaratibu wa chakula utatolewa na kamati ya wazazi. Mwanafunzi afikapo shuleni awe na sahani ya bati, kikombe cha bati na kijiko kwaajili ya chakula awapo hapa shuleni.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kuwa Na .10 ya mwaka 1975 .Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni ukiwa nyumbani (**PREPARATION**)
4. Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira shule
7. Kuvaa **SARE YA SHULE** wakati wote unaotakiwa
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
9. Kutunza mali za **UMMA**

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE AU
KUSIMAMISHWA MASOMO**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika
5. Kupigana na kupiga mwingine
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
7. Kudharau BENDERA YA TAIFA kwa makusudi
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kumpa mwingine ujauzito
9. Kuo au kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kupoteza amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0

**MAMBO MENGINE YA MUHIMU YAKUPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA
MWANAFUNZI ANAPOKUJA KURIPOTI SHULENI**

1. MEDICAL EXAMINATION FORM ambayo inajazwa na MGANGA MKUU wa hospitali ya serikali fomu hiyo itakabidhiwa kwa MKUU WA SHULE mara utakaporipoti shuleni.
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo ,fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
4. Vifaa vya chakula ni sahani ya bati, kikombe na kijiko.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU KYUU SEKONDARI

.....
C. B. KILEO

MKUU WA SHULE

**MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KYUU
S.L.P.175 HAI.**

**OFISI YA RAISI-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
SHULE YA SEKONDARI KYUU
AHADI YA UTII**

A. Ahadi ya mwanafunzi

Miminakubali kupokea nafasi hii ya masomo katika shule ya Sekondani KYUU niliyopewa na serikali. Naahidi kuwa mtii wa sheria zote za shule, nitakuwa mwaminifu , nitajitahidi kujifunza kwa bidii na kwa kadri ya uwezo wangu na kufanyakazi nyinginezo nitakazopangiwa kwa juhudi na maarifa.

NB: Kushindwa kwangu kutii ahadi hii, kanuni na sheria za shule zichukue mkondo wake

Saini ya mwanafunzi.....

Anuani ya nyumbani.....

.....

B. Ahadi ya mzazi/mlezi

Mimi..... nimekubali kumpatia mwanangu (jina la mwanafunzihusika).....mahitaji yote muhimu ya shule (sare ya shule,madaftari,kalamu,vifaa vingine vitakavyohitajika shuleni n.k)ili aweza kujifunza bila matatizo. Naahidi pia kushirikiana na walimu katika kumlea , kumhimiza kujifunza na kufuata sheria za shule na kumhudumia kadiri ya uwezo wangu.

NB: Kushindwa kwangu kutimiza ahadi hii ,kanunu na sheria za nchi na za shule zichukue mkondo wake.

Saini ya mzazi/mlezi.....

Anuani.....

.....

SIMU:.....

PRESIDENT'S OFFICE -RALG
HAI DISTRICT COUNCIL
KYUU SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(This form should be filled by the government medical officer)

STUDENT'S FULL NAME:.....

AGE:.....

BLOOD COUNT (RED AND WHITE).....

STOOL:.....

URINE:.....

V.D:.....

T.B:.....

EYES:.....

EARS:.....

TEETH:.....

SKIN:.....

TREATMENT GIVEN (If any).....

.....

ABDOMEN.....

HEART.....

ANY ADDITIONAL INFORMATION eg.Physical defect,infectious,impairments and any other abnormalities.....

.....

I certify that the above examinee is fit

SIGNATURE:.....